Jinsi ya Kubaini ikiwa Unatimiza Msharti ya Kupata UNM Care au Out-of-County Care

Je, UNM Care na Out-of-County Care ni nini?

UNM Care na Out-of-County Care ni mipango inayowasaidia watu kulipa bili zao za matibabu za UNM Hospital. Huenda ukatimiza masharti ya kuandikishwa katika mipango hii. UNM Care ni ya watu wanaoishi katika Kaunti za Sandoval au Bernalillo. Out-of-County Care ni ya watu wanaoishi katika kaunti nyingine za New Mexico (NM). Ukitimiza masharti, unaweza kupata usaidizi wa kulipia gharama zako za matibabu na huduma za afya katika Hospitali na kliniki za UNM.

Je, Unatimiza Masharti ya Kupata UNM Care au Out-of-County Care?

Kwanza, unahitaji kujua ukubwa wa kaya yako na mapato ya **jumla** ya kila mwezi ya kaya yako. Kisha unaweza kutumia jedwali lililo hapa chini kubaini ikiwa unatimiza masharti.

Ukubwa wa Kaya (Idadi ya watu wanaoishi nawe katika nyumba au fleti moja)	**Mapato ya Jumla ya Kila Mwezi ya Kaya** (Jumla ya kiasi cha pesa kinachochumwa **kila mwezi** na kila mtu katika kaya yako, kabla ya kodi au makato kukatwa)
1	$0 hadi $3765
2	$0 hadi $5110
3	$0 hadi $6455
4	$0 hadi $7800
5	$0 hadi $9145
6	$0 hadi $10,490
7	$0 hadi $11,835
8	$0 hadi $13,180

Mapato ya jumla ni kiasi unachopata **kabla ya** kodi na makato mengine kukatwa. Makato mengine yanaweza kuwa pesa ambazo hukatwa kwa ajili ya mambo kama vile mipango ya kustaafu au bima ya afya.

Unahitaji kujua **jumla ya mapato ya kila mwezi** ya kila mtu katika kaya yako. Kisha unaweza kuyajumlisha ili kupata mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya yako.

Jedwali hili lina ukubwa wa kaya wa hadi watu 8 tu. Kwa hivyo, ikiwa kaya yako ina idadi kubwa kuliko hiyo, unahitaji **kuongeza $1345 kwa kila mtu wa ziada**.

Kwa mfano, ikiwa ukubwa wa kaya yako ni watu 9, unapaswa kuongeza **$1345** kwenye $13,180 (kiasi cha juu zaidi kwa kaya ya watu 8). Ikiwa ukubwa wa kaya

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Je, Unatimiza Masharti — imeendelezwa

yako ni watu 10, unapaswa kuongeza **$1345** nyingine zaidi ili kupata kiwango cha $0 hadi $15,870. Na kuendelea.

Je, Unahitaji Usaidizi wa Kubaini ikiwa Unatimiza Masharti?

Hakuna tatizo—tunaweza kukusaidia! Fuata tu hatua zilizo hapa chini.

Hatua ya 1

Hatua ya kwanza ni kujua ukubwa wa kaya yako. **Ukubwa wa kaya** ni idadi ya watu wanaoishi nawe.

Hali ya 1

Ikiwa una umri wa miaka **18 au zaidi**, kaya yako inaweza kujumuisha watu hawa—

- Wewe
- Mume/mke wako
- Wategemezi wako. Huyu anaweza kuwa mtoto au jamaa ambaye unadai kuwa ni mtegemezi katika fomu zako za kodi. Katika mipango hii miwili, mtegemezi lazima awe anaishi nawe ili kuhesabiwa kama sehemu ya kaya yako. Mtegemezi ni mtu unayemtunza na kukimu mahitaji yake ya kifedha—unalipia chakula, nyumba, nguo na masomo yake, kwa mfano.

  Kuna masharti maalum ambayo hukuruhusu kudai kuwa mtu ni mtegemezi. Ikiwa una maswali kuhusu iwapo mtu katika kaya yako ni mtegemezi au la, tafadhali tujulishe.

Kwa mfano, tuchukulie kwamba unaishi na mume/mke wako na watoto 2. Hiyo inamaanisha kuwa kuna watu 4 katika kaya yako. Ukubwa wa kaya yako ni 4.

Hali ya 2

Ikiwa una umri wa **chini ya miaka 18**, kaya yako inaweza kujumuisha watu hawa—

- Wewe
- Wazazi au walezi wako
- Ikiwa wazazi au walezi wako wana **wategemezi**, unapaswa kuwahesabu pia. Inaweza kuwa ndugu (kaka au dada) au jamaa mwingine anayeishi nawe pia.

Kwa mfano, tuchukulie kwamba unaishi na mama na baba yako na kaka yako mdogo. Kaka yako ni mtegemezi wa wazazi wako. Kwa hivyo, unahitaji kumhesabu kaka yako pamoja na wewe na mama na baba yako. Ukubwa wa kaya yako ni 4.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Kubaini ikiwa Unatimiza Masharti, Hatua ya 2 — imeendelezwa

Hatua ya 2

Hatua inayofuata ni kujua mapato ya jumla ya kaya yako. **Mapato ya kaya** ni kiasi cha jumla cha pesa ambazo kila mtu katika kaya yako hupata. Lakini kuwa mwangalifu—tunataka kiasi cha mapato ya **jumla**, sio mapato halisi.

Mapato ya jumla ni kiasi unachopata **kabla ya** kodi na makato mengine kukatwa. Makato mengine yanaweza kuwa pesa ambazo hukatwa kwa ajili ya mambo kama vile mipango ya kustaafu au bima ya afya. Unahitaji kujua **mapato ya jumla ya kila mwezi** ya kila mtu katika kaya yako. Kisha unaweza kuyajumlisha ili upate kiasi cha mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya yako.

Watu wa kaya yako, ukiwemo, wanaweza kupata pesa (mapato) kutoka kwa chochote kati ya vyanzo hivi—

- ✓ Kazi (ujira, mshahara)
- ✓ Malipo ya ufadhili wa kutokuwa na ajira
- ✓ Malipo kutoka mpango wa Social Security
- ✓ Malipo ya wanajeshi wastaafu
- ✓ Malipo kutoka Bureau of Indian Affairs

Kukokotoa Jumla ya Mapato ya Kila Mwezi ya Kaya

Hebu tutumie familia yetu ya mfano tena—tuchukulie kwamba unaishi na mama na baba yako na kaka yako mdogo. Na tuchukulie kwamba kila mtu anapata kiasi hiki kwa mwezi katika kaya yako. (Kumbuka, hiki ni **kiasi cha jumla**.)

- Unapata $1100 kutoka kwa kazi yako.
- Kaka yako anapata $0.
- Mama yako anapata $4000 kutoka kwa kazi yake.
- Baba yako anapata Malipo ya Wanajeshi Wastaafu ya $2400.

Ukijumlisha malipo hayo utapata **$7500**. Hayo ndiyo mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya yako.

Hatua ya 3

Hatua ya mwisho ni kuona ikiwa unatimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care. Ikiwa unajua **ukubwa wa kaya yako** na **mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya yako**, unaweza kubaini ikiwa unatimiza masharti.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Kubaini ikiwa Unatimiza Masharti, Hatua ya 3 — imeendelezwa

Katika hatua hii, unahitaji kurejelea Jedwali la Ukubwa wa Kaya. Ikiwa unakumbuka familia yetu ya mfano, ukubwa wa kaya yao ni **4** na mapato yao ya kila mwezi ya kaya ni **$7500**. Hebu tuone ikiwa wanatimiza masharti ya kupata UNM Care.

Hivi ndivyo unavyofanya hivyo –

1. Tazama jedwali tena.
2. Tafuta nambari 4 kwenye safuwima ya kushoto ya jedwali (Ukubwa wa Kaya).
3. Tumia kidole chako kufuatilia safumlalo hadi kwenye safuwima ya kulia (Mapato ya Jumla ya Kila Mwezi ya Kaya).

Ndani ya kisanduku kilicho katika safuwima ya kulia, unapaswa kuona **$0 hadi $7800**. Hicho ndicho kiwango cha mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya yenye watu 4. Mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya ya familia yetu ya mfano ni $7500. Kiasi hicho kinalingana na kiwango cha kaya ya watu 4, kwa hivyo wanatimiza masharti!

Ukubwa wa Kaya (Idadi ya watu wanaoishi nawe katika nyumba au fleti moja)	Mapato ya Jumla ya Kila Mwezi ya Kaya (Jumla ya kiasi cha pesa kinachochumwa **kila mwezi** na kila mtu katika kaya yako, kabla ya kodi au makato kukatwa)
1	$0 hadi $3765
2	$0 hadi $5110
3	$0 hadi $6455
4	$0 hadi $7800
5	$0 hadi $9145
6	$0 hadi $10,490
7	$0 hadi $11,835
8	$0 hadi $13,180

Ungependa Kupata Taarifa Zaidi?

Kwa taarifa zaidi kuhusu UNM Care na Out-of-County Care, tafadhali tembelea tovuti yetu—

https://unmhealth.org/patients-visitors/billing-insurance/patient-financial-assistance.html

Bado Una Maswali?

Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali pigia simu kitengo cha Usaidizi wa Kifedha cha UNM kwa **505 272-2521.**

Baada ya kujua ukubwa wa kaya **yako** na mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya **yako**, unaweza kutumia jedwali **kuona ikiwa unatimiza masharti** ya kupata UNM Care au Out-of-County Care. Ikiwa unatimiza masharti, unaweza kupata usaidizi wa kulipia gharama zako za afya na za matibabu za UNM Hospital kupitia UNM Care au Out-of-County Care.